



TAARIFA KWA UMMA

KUFUNGULIWA KWA AWAMU YA TATU YA UDAHILI WA SHAHADA YA KWANZA KATIKA TAASISI ZA ELIMU YA JUU NCHINI KWA MWAKA WA MASOMO 2021/2022

Dar es Salaam, Tarehe 17 Septemba, 2021

1.0 UTANGULIZI

Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU) inapenda kufahamisha umma na wadau wa Elimu ya Juu nchini kuwa Awamu ya Pili ya Udahili kwa ngazi ya Shahada ya Kwanza katika Taasisi za Elimu ya Juu nchini kwa mwaka wa masomo 2021/2022 umekamilika. Majina ya waombaji waliodahiliwa katika Awamu ya Pili yanatangazwa na vyuo husika.

2.0 WAOMBAJI WALIODAHILIWA KATIKA CHUO ZAIDI YA KIMOJA

Waombaji waliodahiliwa katika chuo zaidi ya kimoja katika Awamu ya Kwanza na ya Pili wanahimizwa ***kuthibitisha udahili wao katika chuo kimojawapo kuanzia tarehe 18 hadi 24 Septemba, 2021*** kwa namba maalum ya siri iliyotumwa kwa ujumbe mfupi kupitia namba zao za simu au barua pepe walizotumia wakati wa kuomba udahili. Wale ambao hawatapata kwa wakati ujumbe huo, wanashauriwa kuingia kwenye mifumo ya udahili ya vyuo walivyodahiliwa na kuomba kutumiwa ujumbe mfupi wenye namba maalum ya siri ili kuweza kujithibitisha katika chuo husika.

Uthibitisho wa udahili ufanyike kupitia akaunti ambayo muombaji alitumia wakati wa kuomba udahili. Orodha ya majina ya waombaji waliodahiliwa katika chuo zaidi ya kimoja imewekwa katika tovuti ya TCU (www.tcu.go.tz).

3.0 KUFUNGULIWA KWA AWAMU YA TATU YA UDAHILI 2021/2022

Tume inatangaza kuwa Awamu ya Tatu ya Udahili wa Shahada ya Kwanza kwa mwaka wa masomo 2021/2022 inaanza ***tarehe 18 hadi 24 Septemba, 2021***. Tume inasisitiza kuwa waombaji ambao hawakuweza kutuma maombi ya udahili au hawakudahiliwa katika Awamu zilizopita kutokana na sababu mbalimbali watumie fursa hii vizuri kwa kutuma kwa usahihi maombi yao ya udahili kwenye

vyuo wanavyovipenda.

4.0 WITO KWA WAOMBAJI UDAHILI NA TAASISI ZA ELIMU YA JUU NCHINI

Waombaji udahili wa Shahada ya Kwanza wanakumbushwa kuwa masuala yote yanayohusu udahili au kujithibitisha katika chuo kimoja yawasilishwe moja kwa moja kwenye vyuo husika. Kwa wale ambao watapata changamoto katika kujithibitisha au kutaka kubadilisha uthibitisho wao, vyuo vyote vimeelekezwa kupokea taarifa zao na kutafuta ufumbuzi wa haraka kwa kuzingatia miongozo na taratibu zilizowekwa. Hivyo, wawasiliane na vyuo wanavyotaka kujithibitisha kupitia madawati yao na vyuo vitapokea taarifa zao na kuzifanyia kazi.

Tume inaelekeza Taasisi zote za Elimu ya Juu nchini zinazofanya udahili wa Shahada ya Kwanza kuendelea kutangaza programu ambazo bado zina nafasi na kuzingatia sheria, kanuni na miongozo katika zoezi la udahili ili kuepuka usumbufu usiokuwa wa lazima kwa waombaji udahili na wananchi kwa ujumla.

Imetolewa na:



Dkt. Kokuberwa Katunzi-Mollel
Kny: KATIBU MTENDAJI
TUME YA VYUO VIKUU TANZANIA